# FAIDA YA TANO YA KUFA NA KISHA KUFUFUKA KWA BWANA WETU YESU KRISTO NI KUREJESHA FURAHA, AMANI PAMOJA NA USHIRIKA WETU NA MUNGU AMBAO ULIKUWAUMEPOTEA KWA SABABU YA DHAMBI

## MAANDIKO: LUK. 15: 21-24, MATH. 28:5-10 NA ISAYA. 9:6.

1. Eneo la furaha na amani katika maisha ya mtu aliyeokoka ni eneo muhimu sana na kubwa mno; mtu yeyote anapokuwa hana furaha na amani, hata vitu vingine vyote alivyonavyo vinakuwa bure na visivyo na maana yoyote kwake.

   **Furaha maana yake ni nini hasa Kibiblia?**
   **Furaha – ndani ya wokovu halisi katika Kristo Yesu kumefungashwa na furaha ( Ni ile amani ya ndani sana moyoni mwa mtu ambayo Roho Mtakatifu anaiweka mwenyewe ndani ya mioyo yetu. Gal. 5:22.**

- **Baada ya kuokoka na kisha kujazwa na Roho Mtakatifu, wakati wote Roho Mtakatifu anakuwa analeta ndani yetu hisia nzito ya uwepo wa Mungu na ukaribu wa msaada wake katika maisha yetu hata kama tungekuwa tunapitia katika hatari za namna gani.**
- **Mungu anatiririsha furaha ndani ya mtu aliyeokoka hadi mataifa wanabaki wakimshangaa. Rum. 15:13.**
- **Kila unapokumbuka tu neema ya Yesu kukuokoa na kukufanya mwanae, furaha isiyoelezeka inatiririka ndani ya moyo wako na nguvu ya kumtumikia inaongozeka zaidi; hii ndiyo maana hasa ya kufurahi katika Bwana.**
- Yesu alipoteswa pale msalabani hadi kuuawa wanafunzi wake wote walimwacha; hawakuwa na ujasiri tena wa kumshuhudia **(Math. 26: 69-75),** wengine waliamua kurejea kazi zao, na kama Yesu asingefufuka wangerejea katika dini zao kabisa, hawakuwa na furaha wala amani yoyote; walikuwa wanaona aibu na kujificha, lakini mara tu baada ya wanawake (wanafunzi) kupata habari kwamba Yesu hayuko kaburini amefufuka kama alivyosema mlipuko wa furaha kuu ukatoka ndani yao- **Math. 28:5-10* mst. 8.** ***Ampl. Bible says- So they left the tomb hastily with fear and great joy and ran to tell the disciples.***

- Kama kuna tendo kubwa katika Biblia lililo wainua mno wanawake na kuwapa heshima kubwa mbele za Mitume na mbele za Mungu; ni tendo hili la kufurahi furaha Kuu na kushangilia kufufuka kwa Bwana Yesu wakati Mitume (Wanaume) bado walikuwa wamejikunyata na kutilia shaka kufufuka kwa Bwana Yesu. ***Luk. 24: 6-12.***
- **Huu ni ukweli uliogeuza kabisa dhana iliyokuwa imejengeka kwamba ukweli wa Mungu lazima upitie kwa wanaume kwanza na kisha wanaume wawafikishie wanawake baadaye; Ni wanawake waliomwona kwanza Yesu alipofufuka na Yesu akajidhihirisha kwao kwanza na kisha wanawake ndiyo wakawapelekea habari za kufufuka kwa Yesu kwa wanaume na kuwapa maelekezo wapi waende ili Yesu akutane nao huko!!! Yoh. 20: 14 – 18, Math. 28: 5 – 10.**
- **Huyu ndiye Yesu mwanaume wa wanaume ambaye ana mamlaka ya kupinduapindua desturi zetu za kibinadamu na kisha kuweka heshima juu ya watumishi wote wa Mungu wawe wa kiume au wa kike**.

**Note**: **Math. 28:8 (Wakaondoka upesi kutoka kaburini, kwa hofu na furaha nyingi, wakaenda mbio kuwapasha wanafunzi wake habari) maana yake walifurahia sana habari waliyopewa kwamba Yesu amefufuka, lakini bado walikuwa na maswali wakijiuliza amekwenda wapi hadi Yesu alipowatokea na wakakaribia na kumshika miguu na kisha wakamsujudia (Math. 28:9); Najaribu kuzumu katika ufahamu wangu siku hiyo jinsi hawa wanawake walivyokuwa wakifurahi; wakitamba katika mitaa yao nashindwa kupata maana hadi Biblia iandike wakafurahi kwa furaha kuu siyo mchezo, na mwanamke akifurahia jambo hata kama wewe ni Mfalme unaona ufalme wako hauna maana tena. 1Samwl. 18: 6 – 9. (Tuone furaha pia ya hawa wanawake wa Israel.**

- Unajua hawa wanawake kutoka Israeli yote walitoka ili kulikaribisha nyumbani jeshi lao la Israel lililokuwa limeshinda majeshi ya Wafilisti. Furaha yao kwa jeshi lao lililorudi salama ilionyeshwa kwa njia ya kuimba na kucheza; wao waliimba na kucheza kwa mioyo ambayo haikuwa na hila ya aina yoyote na kamwe wasingetegemea kwamba Mfalme Sauli angetafsiri maneno yao kama alivyoyatafsiri; lakini ilikuwa ni haki kabisa kwa Daudi aliyejitosa kukabiliana na Goliathi kupongezwa kwa nyimbo!!! Wanawake hawa waliimba kwa msukumo toka moyoni, kushindwa kwa Goliathi na jeshi lote la Wafilisti kulirejesha heshima ya Mungu.
- **Ona pia kushinda kwa Mungu wakati majeshi ya Misri yalipozama kilindini mwa bahari na mizoga yao kuelea ufuoni mwa bahari baadaye**; kuliamsha furaha na shangwe na kucheza kusiko kwa kawaida kwa Taifa lote la Israeli walioshuhudia tendo hili wanawake wakiongoza kwa kuimba na kucheza!! **Kut. 15: 1 – 21* 20-21.**

- Wanaimba na kucheza wakitaja ukuu wa Mungu pamoja na ushindi wake mkuu dhidi ya majeshi ya adui **(kut.15:3–19); Najaribu ku-zumu siku hii pia jinsi ilivyokuwa kwa Wana wa Israeli nashindwa kupata picha yake kamili ya furaha yao jinsi ilivyokuwa; haielezeki!!! Naonaga tambo za Wana wa dunia pale timu yao inaposhinda na kutwaa kombe. Wanakimbizana magari hovyo, mapikipiki n.k. ushindi ni kitu kinachofurahisa mno.**

**Sasa:** Kushinda kwa Bwana Yesu dhidi ya shetani na majeshi yake lazima kuamshe furaha na shangwe kubwa ndani ya kila mteule aliyeokoka na kufahamu kwa kina kazi aliyoifanya Mwokozi wetu pale msalabani. ***Kolos. 2: 13-15, Efes. 2: 1 -15, Ufun. 1: 17 – 18.***

- Kweli kabisa ukijikuta unasema kwamba umeokoka lakini unaishi bila furaha wala amani eti kwa sababu una jaribu Fulani au dhiki Fulani au shida Fulani, wewe unahitaji kutokewa na Yesu kwa upya **– Yak.1: 2-4, Mdo.5: 40-42, Mdo.16:19-34* 25, Rum. 5:3**.

***Note*:Tunapojaa furaha na amani wakati wote kutokana na kazi aliyoifanya Yesu Kristo pale Msalabani zaidi ya miaka 2000 iliyopita; tunamfanya Mungu aachilie Baraka na neema ambazo kamwe hatukustahili kuwa nazo**.

- **Ngoja nimalize ujumbe wangu huu leo kwa kuwaambia wazi kwamba "Wokovu huu tulio nao ndiyo ambao umetuvika heshima ambayo kwa kweli hatukustahili kabisa (eti leo tunalindwa na majeshi ya Malaika) Zab. 34:7, 2Wafal. 6: 16-17, Dan. 6: 22 n.k. eti leo Yesu amenipa mamlaka ya ajabu sana mbele za shetani ya kutamka aondoke na anaondoka pamoja na kiburi chake chote alichonacho!! Luk. 10:19, Zek. 3: 1-7!!n.k. Tangu siku ulipookoka tu; tukio kuu la kwanza lililofanyika juu Mbinguni ni Furaha – Luk. 15: 10 -24.**
- Ndiyo sababu Mtume Paulo aliwahimiza sana Wafilipi wafurahi sana katika Bwana wakati wote- **Filip. 4:4** na **Nabii Isaya** anawasihii hata wasiozaa na wasioolewa wapaze sauti zao za furaha kwa Bwana kwa sababu ya tendo moja tu kubwa la kuchaguliwa na Bwana – ***Isay. 54: 1 – 3.***
- Mwana mpotevu aliporejea kwa Baba yake, akavuliwa mavazi ya hovyo na kuvikwa mavazi ya heshima na viatu miguu, sherehe ilianza, kukawa furaha kuu!! Bwana Yesu asababishe furaha kuu ndani ya kila mmoja siku hii ya leo. **Amina.**

***Na***
***Askofu Dr. L.M. Mwizarubi***
***24/04/2022***